JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO

Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb. Na. DED/NMT/C.50/7/44 20 Julai, 2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kupitia Kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na.FA.170/367/01 "TEMP"/8 cha tarehe 24 Juni, 2021 kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Anatangaza nafasi za kazi kwa wananchi wa Tanzania wenye sifa na ujuzi wa kujaza nafasi zifuatazo:-

1: Mtendaji wa Kijiji Daraja la III (Nafasi 3)

(a) Sifa za Mwombaji:

- Awe amehitimu Kidato cha nne au sita na cheti cha mafunzo (**NTA LEVEL 5**) katika fani mojawapo kati ya hizi; - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii (Sociology). Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

(b) Kazi na majukumu ya Mtendaji wa Kijiji Daraja III

Mtendaji wa Kijiji atatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa Raia na Mali zao,
- Mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji,
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo kijijini,
- Katibu wa Mikutano Mikuu na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji,

- kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika ngazi ya Kijiji.

(c) Ngazi ya Mshahara:

- Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III atalipwa mshahara ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

2: Katibu Mahsusi Daraja la III (Nafasi 1)

(a) Sifa zinazohitajika.

- Muombaji awe amehitimu Kidato cha nne,
- Awe amehitimu mafunzo ya uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu,
- Awe amefaulu somo la Hati Mkato ya Kiswahili na Kingereza mamneno themanini (80) kwa dakika moja,
- Awe amepata na kufaulu mafunzo ya Kompyuta katika Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na awe amepata cheti katika progaramu za Windows, Microst Office Packages na Internet, email na Publishers.

(b) Kazi na Majukumu yake:

Katibu Mahsusi Daraja la III atafanya kazi/majukumu yafuatayo;-

- Kuchapa taarifa, barua na nyaraka mbalimbali za kawaida
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu za kuhudumiwa,
- Kusaidia kutunza taarifa, kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za Vikao, safari,
- Kusaidia kutafuta majalada na kumpatia Mkuu wake kwa kwa wakati unaohitajika,
- Kusaidia kupokea majalada na kuyagawa kwa maafisa walio katika sehemu alipo na kukusanya na kuyatunza katika sehemu husika.

(c) Ngazi ya Mshahara:

- Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Katibu Mahsusi Daraja la III atalipwa mshahara ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

3: Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II (Nafasi 1)

(a) Sifa zinazohitajika

- Muombaji awe amehitimu Kidato cha nne au sita,
- Awe amehitimu na kufaulu ngazi ya Cheti cha utunzaji wa Kumbukumbu (**NTA LEVEL 5**) katika mojawapo wa fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

(b) Kazi na majukumu ya Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja II

- Kuweka kumbukumbu (nyaraka na barua mabalimbali) katika majalada,
- Kutafuta kumbukumbu,nyaraka, majalada yanayohitajika na watumiaji,
- Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka zinazo ingia na kutoka nje ya Taasisi,
- Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi,
- Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.

(c) Ngazi ya Mshahara:

- Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la III atalipwa mshahara ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

4: **MASHARTI YA JUMLA**

(i) Barua za maombi ziambatishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma, Cheti cha kuzaliwa Cheti au namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) vilivyothibishwa na Wakili au Mahakama,

(ii) Mwombaji ambatishe Picha mbili za rangi (Passport Size) za hivi karibuni,

(iii) Kwa wale waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kwamba vyeti vyao vimehakikiwa na kuthibitishwa na Mamlaka (TCU au NECTA) kulingana na ngazi ya cheti,

(iv) Maombi yaambatishwe na maelezo binafsi (CV),

(v) Mwombaji awe na umri wa miaka 18 hadi 45

Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kupitia Posta kwa anuani ifutayo;-

Mkurugenzi Mtendaji (W),

Halmashauri ya Wilaya Namtumbo,

S. L. P 55,

NAMTUMBO.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10 Agosti, 2021 saa tisa alasiri.

NB: Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.namtumbodc.go.tz

Evance Nachimbinya

Mkurugenzi Mtendaji (W)

NAMTUMBO

MKURUGENZI MTENDAJI (W) 22 JUL 2021 P.O. BOX 55 HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO